ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki

11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera

22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa

39. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake

80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Sita - Tarehe 10 Juni, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 61

Utengenezaji wa Jahazi Maalum kwa ajili ya Wageni wa Mhe. Rais

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kidogo swali langu hili liliendana sambamba na swali ambalo nimeuliza, kuhusiana na serikali kujenga kwa upande wa fukwe wa upande wa Ikulu ya Mnazimmoja kutengeneza uzio au *jetty*. Kwa vile serikali ilikiri kwamba hawako tayari kwa ajili ya kuweka *jetty*. Hivyo, swali langu hili la wageni wa Rais jahazi maalum litakuwa liko *invalid*. Kwa hiyo, kwa heshima kabisa naomba niliondoe. Ahsante sana. *(Makofi)*

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Said. Katibu kwa wizara inayofuata.

Nam. 183

Kucheleweshwa Kuchukuliwa Hatua kwa Wanaovunja Sheria

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi niungane na Mhe. Simai Mohammed Said kwa maslahi mafupi na kukiri kwa swali hili litafanyiwa kazi. Naomba nimwambie tu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na Mhe. Naibu Waziri wake watulie wakae kwenye viti wala wasije wakaenda mbele. Naomba kuliondoa. *(Makofi)*

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Katibu kwa wizara inayofuata.

Nam. 173

Ukosefu wa Ajira kwa Vijana Wanaomaliza Vyuo Vikuu

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar imekuwa na vijana wengi wanaomaliza vyuo vikuu katika fani mbali mbali, lakini vijana hao wanapomaliza wanakosa fursa za ajira. Lakini cha kusikitisha serikali imekuwa ikiwaongezea mikataba ya ajira wafanyakazi ambao wameshafikia umri wa kustaafu wakati vijana wa kushika nafasi hizo wapo na wananyimwa ajira kwa kisingizio cha uzoefu na umri na uchache wa nafasi za ajira.

(a) Je, ni sababu gani zinapelekea watu waliostaafu kupewa mikataba ya kazi wakati vijana wanaomaliza vyuo katika fani hizo wapo.

(b) Kuna watu wangapi wameongezewa mikataba ya ajira na fani zao ni zipi.

(c) Kuna tathmini gani imefanywa kujua vijana ambao hawana ajira na fani zao ni zipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 173 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Uajiri wa Mkataba katika Utumishi wa Umma Zanzibar upo kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 60 (1) (b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi makini swali lake kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, sababu za msingi zilizopelekea kutoa mikataba kwa wastaaafu ni upungufu wa wataalamu katika sekta husika. Aidha, kifungu cha 8 cha Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 5 ya 2012, kinampa uwezo Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma, kuhusu ajira ya mikataba kwa mtaalamu husika kwa kutangaza fani hizo katika Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hatua hii itaendelea hadi serikali itakapojitosheleza kitaalamu katika fani mbalimbali.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2011 – 2017 jumla ya watumishi mia moja na tatu (103) wamepewa ajira ya mkataba wa muda maalum wa utumishi na fani zao kama notisi ilivyoelekeza ni waalimu wa Sayansi, Hesabati, Madaktari wa Binadamu na Wanyama, Wataalamu wa Uchumi na kadhalika.

(c) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya kujua vijana ambao hawana ajira, shughuli hizo kwa mujibu wa taratibu zinafanywa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Hatahivyo, kwa kumbukumbu za hivi karibuni ni kwamba vijana wengi waliosomea fani ya sheria na utawala ndio ambao wamekosa ajira zaidi kutokana na ufinyu wa nafasi hizi katika soko la ajira nchini. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya serikali naomba kuuliza swali dogo tu.

(a) Kwa nini serikali wanawapa ajira za mikataba watu waliostaafu wakati vijana wenye fani kama zao wako mitaani wakiwa hawana ajira pamoja na kuhitimu elimu za juu.

Ni sababu gani, kwa mfano hata hili swali la pili alipojibu wengine hakuwajata humu na ushahidi na watu wapo.

(b) Lakini hii idadi aliyoitaja ya 103 Unguja tuu au pamoja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu mama swali la ajira za mikataba hili linafanyika kutokana na sheria ambayo tunayo. Sasa ajira za mikataba zimeruhusiwa kwa mujibu wa sheria, halikadhalika kuwepo kwa ajira za mikataba serikali haizuiliki kuajiri vijana wake ambao wako mitaani, tunafanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo kuwaajiri

vijana wetu mbalimbali pale ambapo tutakuwa na nafasi zinazohitajika.

Sasa na pale ambapo serikali tutakuwa na mahitaji maalum kwa watu maalum ambao wametajwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, basi watu hao tutawaajiri katika yale mahitaji ambayo tunayahitaji kwa sababu hatuajiri tuu au hatuwapi wafanyakazi mikataba kuwaongezea bali panakuwa pana mahitaji maalum ndipo ambapo tunafanya hivyo.

(b) Kuhusiana na hii takwimu kwamba ni Unguja na Pemba. Nashukuru.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Zanzibar imekuwa na vijana wengi wanaomaliza vyuo kwa fani mbali mbali na kwa kuwa Zanzibar pana upungufu mkubwa wa baadhi ya wizara kwa wafanyakazi, kwa mfano kama Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya.

(a) Kwa nini serikali haiwaajiri wanafunzi hawa wanaomaliza vyuo baadae wanakwenda kuajiriwa Tanzania Bara na upungufu hapa upo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar vijana wao wanaomaliza vyuo mbali mbali nchini na nje za nchi inawaajiri pale ambapo tunakuwa na nafasi. Sasa tukisema kwamba

wanaajiriwa Tanzania Bara sisi hatuwaajiri, si sahihi inawezekana wanaajiriwa huku anakosema, lakini na sisi tunaajiri. Kwa taarifa tu tulikuwa na suala zima la wahitimu wa vyuo vikuu katika suala la elimu. Sasa kulikuwa na upungufu wa walimu wa sayansi ajira za walimu wa sayansi na Mhe. Mwenyekiti yeye Mwakilishi ni shahidi kwamba tumewaajiri watu wengi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa tu kuna watu ambao walioajiriwa Tanzania Bara wanatoka kule kuja huku kufuata ajira na hususan katika walimu wa sayansi. Sasa tunaajiri na tutaendelea kuajiri kila pale ambapo tutakuwa na uwezo kuajiri vijana wetu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake na kukidhi kuwa wapo wafanyakazi wameajiriwa kwa mikataba. Lakini ukiangalia swali la msingi na maelezo ya Mhe. Waziri aliyejibu kidogo pana utata ndani yake hasa ukizingatia serikali inaishi kwa kuzingatia mipango na tafiti mbali mbali hasa kupitia hizi Idara za Rasilimali Watu. Kwa kuwa wanajua siku ambayo mtaalamu anaanza kazi na kujua siku mtaalamu huyo anamaliza kazi kwa maana siku yake ya kustaafu.

(a) Kwa nini serikali kupitia hizi Idara ya Rasimali Watu haziwa-*train* wafanyakazi kwa kuzingatia zile sifa na kuona siku ambazo wafanyakazi wengine wanastaafu.

(b) Kuendelea kufanya hivyo, kutowa-*train* na wakati tafiti n mikakati mbalimbali ya serikali inaelewa wataalamu gani wanastaafu na siku fulani, kwa idara zetu zinaendelea kuishi bila kufanya kazi kwa ufanisi na kufanyakazi wa mazowea.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu serikalini tunao wa ku-*train* wafanyakazi wetu kwasababu tunao mpango tunauita *Succession Plan*, mpango huu tunaufanya makazini mwetu, maidarani mwetu kuhakikisha kwamba wale ambao wanaokuwepo basi wanakuwa wanajifunza kwa kile ambacho wale ambao watakaostaafu wanawaachia wao. Kwa maana ya kwamba watakapoandoka wale wanaostaafu basi na hawa ambao wapo katika kazi huwa wanapata kujifunza mambo zaidi.

Kwa hivyo, mpango huo tunao Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwa jawabu hilo la (a) naona hakutokuwa na sababu ya kujibu (b) kwa sababu itakuwa tayari limeshajitosheleza.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana aliyoyajibu. Lakini pia naomba kuongeza kidogo kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake linalohusiana na je, hatuna *data* za kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuthibitishieni kwamba Wizara yetu ya Utumishi hivi sasa mtu kama anastaafu baada ya miezi sita, basi huwa tunatoa barua *in advance* kumjulisha kwamba ikifika tarehe fulani itakuwa muda wako wa utumishi serikalini umemalizika. Kwa hivyo, taarifa zipo na *data* zipo serikali hii ni makini asiwe na mashaka.

Nam. 112

Uzalishaji wa Chakula Zanzibar

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi kutoa huduma na mafunzo kwa bibishamba na bwanashamba, ili eneo dogo litumike na kupata mazao mengi zaidi, lakini wizara hii ina maeneo mengi inayoyamiliki lakini maeneo hayo yamesahaulika.

(a) Kwa kuwa wao ni wataalamu wa kilimo (bibishamba na bwanashamba) kwa nini hawaoneshi mfano wa uzalishaji bora katika mashamba hayo.

(b) Kwa kuwa wizara hii ina dhamana ya chakula hapa Zanzibar, kwa sasa nchi ipo asilimia ngapi kufikia kujitosheleza kwa chakula.

(c) Mchele ndio chakula kikuu, ni lini Zanzibar itajitosheleza kuzalisha mchele wa aina tofauti.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 112 kama ifuatavyo:-

Awali ya yote naomba kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi haijayasahau maeneo hayo. Wizara yangu inamiliki mashamba ambayo yanatumika kwa ajili ya kazi za utafiti, uzalishaji wa mbegu, uzalishaji mifugo, hifadhi za misitu ya asili na upandaji misitu kwa ajili ya uzalishaji mbao na kuhifadhi mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2013, wizara pia ilipewa jukumu la kuyatambua mashamba yaliyokuwa ya eka yanayokadiriwa kufikia 8,000 katika Kisiwa cha Pemba kwa ajili ya kuyatambua na kuyasimamia hadi hapo serikali itakapoelekeza umiliki mbadala wa mashamba hayo. Wizara yangu pia inasimamia mabonde ya mpunga ambayo yanatumiwa na wakulima kwa ajili ya kilimo cha mpunga wa kumwagilia maji na mpunga wa kutegemea mvua.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo sasa naomba kumjibu swali (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haioni haja ya kuwapatia mabibishamba na mabwanashamba maeneo maalum kwa kazi hiyo. Hii ni kwasababu matumizi ya mashamba ya serikali yaliyo chini ya wizara yangu yanajumuisha utowaji wa elimu kwa wakulima kupitia wataalamu waliopangiwa kazi katika maeneo ya utafiti, uzalishaji mbegu, mifugo na utunzaji misitu. Kwa hivi sasa wataalamu wa kilimo (bibishamba na bwanashamba) wanaonesha mfano wa uzalishaji bora katika mashamba maalum ya mfano katika skuli za wakulima ambayo hufanyika katika mashamba ya wakulima.

(b) Takwimu za mwaka 2016 zinaonesha Zanzibar inajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 60 na asilimia 40 ya chakula kinacholiwa nchini kinaagizwa kutoka nje ya nchi. Hili ni ongezeko la asilimia 11 kutoka mwaka 2005 ambapo kwa wakati huo Zanzibar ilikuwa inajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 49 tu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar hivi sasa inajitosheleza kwa mazao ya muhogo, ndizi na viazi vikuu na vitamu na imepiga hatua kubwa katika kupunguza utegemezi wa matunda na mboga kutoka nje kutoka asilimia 70 mwaka 2006, hadi asilimia 20 mwaka 2016. Chakula pekee ambacho bado uzalishaji wake uko chini ya mahitaji ya nchi ni mchele ambao hivi sasa unakidhi asilimia 20 tu ya mahitaji yetu na asilimia 80 unaoliwa nchini unaingizwa kutoka nje ya nchi.

(c) Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ina nafasi kubwa ya kuongeza uzalishaji wa mchele na kupunguza utegemezi wa chakula hiki kutoka nje ya nchi pale tutakapokamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji na kuanza kuzalisha mpunga kwa mfumo wa umwagiliaji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ifahamike kwamba mabadiliko ya tabianchi yanayoikabili nchi yetu yanaathiri sana sekta ya kilimo na kufanya kilimo cha kutegemea mvua hivi sasa kuwa si cha uhakika. Serikali imeliona hili na inaendelea na jitihada za kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji na kushajiisha matumizi ya teknolojia za kisasa za umwagiliaji wa matone. Hadi hivi sasa hekta zipatazo 800 za mpunga wa umwagiliaji maji ndio zenye miundombinu iliyokamilika.

Mhe. Mwenyekiti, eneo hili linazalisha wastani wa tani 8,100 ambao ni wastani wa uzalishaji wa tani 5 kwa hekta mara mbili kwa mwaka za mpunga ambazo ni wastani wa tani 4,800 za mchele. Katika kipindi cha miaka mitatu ijayo wizara inategemea kuendeleza hekta 1,560 kwa mashirikiano na *Exim Bank* ya Korea na Benki ya Dunia.

Mhe. Mwenyekiti, ongezeko la eneo hili litawezesha kuongeza uzalishaji mpunga kutoka tani 20,652 ambazo ni wastani wa tani

12,400 za mchele, mpango huu utaenda sambamba na utowaji wa ruzuku kwa pembejeo katika mabonde ya umwangiliaji maji wa mpunga wa kutegemeza mvua.

Mhe. Mwenyekiti, katika mabonde ya kutegemea mvua uzalishaji unategemea kuongezeka kutoka wastani wa tani 0.7 kwa heka na kufikia tani 1.5 na kuwezesha uzalishaji wa wastani tani 45,000 elfu za mpunga katika eka ya 30,000 ambazo ni wastani wa tani 27,000 elfu za mchele. Kutokana na takwimu hizi zinaonesha kuwa nchi inaweza kuzalisha tani 44,200 za mchele na kujitosheleza kwa wastani wa asilimia 50 ya majitaji ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, nachukuwa nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi waunge mkono jitihada za serikali kwa kusaidia wakulima katika majimbo yao waweze kupata mitaji, ili waweze kumudu teknolojia za kisasa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri, Waziri mahiri ambaye anajibu kwa ufasaha zaidi nimpongeze sana. Lakini kidogo kwa ufafanuzi pamoja na kupata faida kwa wananchi nataka nimuulize swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa mabwanashamba *profession* yao ni mambo ya kilimo pamoja na mifugo. Je, haoni umuhimu wa kuwapa eneo katika maeneo yako kila *doctor* au bwanashamba akapata kuona elimu yake au utendaji wake umefikia wapi katika kuwagaia mashamba, ili wao najua watakuwa ni miongoni mwa uzalishaji wa kuongeza pato.

(b) Zanzibar tunakula sana nyama ya ng'ombe, lakini ng'ombe hatuna, pia ng'ombe tunaoagiza kutoka Bara wanakuwa lazima watakapokuja hapa wapate pengine chanjo pamoja na kuangaliwa, pengine inaweza kufika

wiki mbili, ili kupata uhakika wa afya yake. Mhe. Mwenyekiti, suala hili tumewaachia wafanyabiashara kwamba wao watuletee ng'ombe, kwa hiyo anapokuja hata kama anachinjwa kwenye boti au sehemu nyengine yoyote ndio anafika watu wanamla.

Kwa wizara yake haoni umuhimu wa kuwa biashara hii akaichukua yeye kutoka Bara yaani *import,* maana yake kutoka Bara akaweza kuwafunga ng'ombe kwa muda ambao kiafya unaweza ukawa-*fit* na wakaliwa salama baadae ukawauzia wafanyabiashara wa hapa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuhusu mabwanashamba na mabibishamba kuwapa maeneo hawa ni waajiriwa na kazi ya kilimo ni kazi ya muda mrefu sana, unapowapa shamba lake na la kwake ile kazi yao ya ajira kwanza itakuwa haipo. Ndio maana tukasema katika maeneo ambayo wanafanya kazi mashamba yale ya skuli ndio yatumike, hayo kama mashamba ya darasa kwa ajili ya wakulima wetu, ukianza kuwapa wao wataacha kazi yao ya msingi ile *core function* wanayotakiwa kuifanya watafanya ile kazi ya kwao. Ni sawa sawa, hata sasa hivi tuna matatizo wakati mwengine madaktari wanakuwa na *private hospital*, hafanyi kazi zake vizuri katika hospitali za serikali anafanya zaidi katika kazi ya binafsi kwa sababu anapata mapato zaidi. Sasa nasema na hili nalo ni vizuri tukaliangalia katika misingi hiyo kwamba tunataka tuone ufanisi wa utendaji, ndio maana tunafanya hivyo, na ndio maana tukafungua mashamba darasa, ili kuweza kutoa taaluma kwa wakulima wetu.

Kuhusu swali la ng'ombe kwamba serikali ichukue biashara. Serikali ukisoma taarifa zote za serikali muongozo wa CCM wenyewe unasema wazi kwamba sekta binafsi ndio muhimili wa uchumi, na tungependa sana sekta binafsi zifanye hizi shughuli.

Mhe. Mwenyekiti, tunachoweza kufanya sisi ambacho tunataka kufanya sasa hivi, shamba letu la Kipange ni kuweka mitamba pale, ili wananchi sasa waweze kupata mitamba mizuri ya kufuga na vilevile waweze kununua na kuweza kufanya biashara zao.

Lakini serikali kama serikali kufanya biashara moja kwa moja haitokuwa jambo zuri, ila tunawahimiza na kwamba kuna *private sector* iko tayari kuwekeza katika hilo tuko tayari kuwasaidia, kuwasaidia kupata mikopo ili wawekeze wafanye hiyo biashara kwa ufanisi nawe ni mtaalamu wa mambo haya karibu uwekeze katika sekta hii.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa ruhusa kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka kumkumbusha Mhe. Waziri msemo wa mwana falsafa maarufu duniani Mahatma Gandhi alisema: *"Realization as a human potential*". Mhe. Mwenyekiti, amesema yeye Mhe. Waziri kwamba hali ya mabadiliko ya hali ya hewa inasababisha upungufu wa ulimaji wa mpunga, lakini pia ajue kwamba Zanzibar chakula tunachokula ni mchele na alituahili hapa ataulima mchele. Je, wizara yake ina mkakati gani wa kulima mpunga wa umwagiliaji maji *atleast* asilimia 50 ya tunachoagiza.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na namshukuru sana Mhe. Mjumbe kwa swali lake kama anafuatilia maelezo ambayo nimeyatoa kwa urefu nimeonesha takwimu ambazo zitatupatia angalau asilimia 50 ya mchele ambao unazalishwa hapa nchini. Tuna mpango na *Exim Bank* ya trekta 1,560 za umwagiliaji maji, tunaanza programu mwaka huu tunategemea katika kipindi cha miaka miwili trekta hizo zitakamilika. Tunazo hekta 800 ambazo

tunafanya *exercise* za kumwagilia maji, lakini vile vile kuna mpango mwengine wa kumwagilia kwa matone ambao tunafanya wa Waisrael kwa ajili ya kumwagilia kwenye matone.

Tunaamini mipango hii tukipata hekta 5,000 asimilia zaidi ya 50 ya mchele itapatikana. Kama alifuatilia majibu niliyoyatoa nimetoa takwimu sahihi za kuonesha ni juhudi gani tunafanya hivi sasa. Mhe. Mwenyekiti, nataka nichukue nafasi hii vile vile kuwashukuru sana wakulima ambao wamekubali kulima Kilimo Shadidi mwaka huu naomba mupite kwenye mashamba muone wakulima walivyofanya kazi vizuri na naamini tukiendelea na juhudi hizi hali ya chakula itabadilika sana ya mchele. *(Makofi)*

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye vipengele (a) na (b).

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na ya ufasaha. Lakini ningependa nimuulize. Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya Mhe. Waziri katwambia hapa kwamba mabwanashamba na mabibishamba hawana haja ya kupewa mashamba mengine kwa ajili ya kuweka haya mashamba ya masomo, lakini pia katueleza kwamba kuna vituo ambavyo vinatolewa mafunzo kwa ajili ya wakulima.

(a) Ningependa atwambie hivi vituo vinavyotolewa haya mafunzo viko kila wilaya au viko katika shehia au viko kwenye utaratibu gani kwa hawa wakulima.

(b) Kwavile hawa mabwanashamba na mabibishamba hawana haja ya kupewa haya mashamba, na hivi vituo ambavyo wakulima wetu wanapatiwa mafunzo na watafiti wapo wanafanya kazi hii kwa ajili ya hawa wakulima. Kuna haja gani ya kuwaweka hawa

mabibishamba na mabwanashamba ambao wameshaajiriwa na wanafanya kazi hii na wanalipwa na mishahara, kwa ajili ya hii ajira yao lakini hizi kazi kama hazina haja kwao za kuzifanya. Je, kuna haja gani ya kuwaweka hawa mabibishamba na mabwanashamba wakati hivi vituo vipo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake la nyongeza lenye vipengele viwili kama ifuatavyo.

Mabwanashamba na mabibishamba wameajiriwa kwa kazi maalum ya kutoa taaluma, na taaluma hii wanaipata kupitia Chuo chetu cha Kizimbani tuna wa-*train* pale na yapo mashamba ya mfano, lakini kila shehia tumejitahidi, baadhi ya shehia kuweka mashamba ya mfano ambao wakulima wenyewe wanayo na tunawafanya kama ndio mashamba darasa. Sasa anaposema waache wasiendele hii ni kazi taaluma ni kazi endelevu, kwa mfano hatukuwa na taaluma ya Kilimo cha Shadidi kama mabwanashamba na mabibishamba tuliwaondoa, maana yake itabidi tuwaajiri watu wapya kwa kuja taaluma mpya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu taaluma ni *process* kusoma ni uendelevu haukomi kusoma hata ukiwa mzee kiasi gani unasoma, sisi wengine wazee tunaendelea kusoma. Mhe. Mwenyekiti, kuna hawa mabwanashamba na mabibishamba watatoka katika *stage* hii wanaweza kuingia kwenye *stage* nyengine wakawa wataalamu wakubwa zaidi baada ya kupata taaluma za msingi ambazo wanazipata, yaani wale mabwanashamba na mabibishamba ni kama taaluma za msingi kwao.

Kwa hiyo kusema uwakatishe uwaondoe maana yake umewakatisha kupata taaluma ya kuendelea, na wengine kwa taarifa yako wameshafanya hata *diploma* sasa hivi wameshatoka katika bibishamba na bwanashamba. Hivyo, hii ni *process* ni vizuri wakaendelea na mimi nawa-*encourage* wajitahidi sana kutumia uzoefu watakaopata pale, ili wajiunge sasa na vyuo wawe more *professions* ambao tunawahitaji kwa wingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwa pamoja maswali haya kwamba nasema kila shehia tunayo mashamba ya mfano. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe katika maeneo yenu mkaangalie utakuta shamba la mfano, shamba darasa la migomba, shamba la darasa la mihogo yako kila pahala tumeyaweka, nafikiri ni vizuri mwende mkaangalie haya yanakuwa *only* yanamilikiwa na wenyewe wakulima, sisi tunatumia kama mashamba ya darasa lakini yanamilikiwa na wakulima wenyewe.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri wa Kilimo.

Mhe. Waziri nikupongeze kwa majibu yako mazuri ambayo umetoa. Lakini swali langu linakuja kutokana na maelezo aliyotoa kabla ya kujibu maswali kwamba imekuwa wizara yake ikifuatilia kuhakiki mashamba ya eka yote nchini katika maelezo yake. Je, tayari anayatambua mashamba ambayo masheha wetu baadhi yao wasio waaminifu wameanza kufanya utaratibu na kuyarejesha mashamba hayo kwa wenyewe wa asili. Mhe. Mwenyekiti, kama anayajua je, ni hatua gani mashamba hayo yamefanywa kiasi ambacho wale ambao wamemilikishwa na serikali wanaendelea kuyamiliki.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Samahani Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na *echo* sikusikia hata kidogo maelezo arudie kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kabla hujajibu, Waheshimiwa Wajumbe tusome na Kanuni ya 61 (e) sauti zinazidi mpaka Mhe. Waziri anashindwa kujibu kwa sababu hasikii, sauti zetu zinatoka sana kuliko hata anayeuliza au anayejibu swali. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe sauti zisipande, ili mumpe nafasi Mhe. Waziri aweze kujibu kwa usahihi na yule anayeuliza apate asikie jibu lake kwa usahihi. Hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kila mtu kwenye kiti akipitie hicho kifungu tumetunga wenyewe hizi Kanuni. Mhe. Mjumbe, naomba urejee swali Mhe. Waziri hakusikia.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yake kabla ya kujibu swali mama alieleza kwamba wizara yake ilikuwa inafanya uhakiki wa mashamba ya eka na wamiliki wao. Je, anajua kwamba kuna baadhi ya masheha ambao si waaminifu wamefanya utaratibu au kama kwa kuahidiwa kupata kitu au kupewa kitu na mashamba yale yakarejeshwa kwa wamiliki wa asili badala ya wale ambao wemepewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, analijua hilo. Sasa kama analijua je, ni hatua gani imechukuliwa dhidi ya wale ambao wamiliki wa asili na wale ambao wamefanya ubadhirifu kuyarudisha mashamba hayo kwa kushirikiana na maafisa wake wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mhe. Mjumbe kwa swali lake zuri sana. Kwanza nataka nikiri kabisa serikali baada ya kubaini kwamba kuna umiliki si wa halali katika mashamba tumechukua hatua mbali mbali, moja ikiwa ni kuunda kamati

yetu sisi ya wizara kupitia na kukagua moja baada ya moja. Kazi hiyo inaendelea haijamalizika na itakapokamilika taarifa tutaitoa.

Lakini upo ukweli kabisa kuna watu wamepewa eka tatu na kwa bahati mbaya wamezitoa kinyume cha sheria. Sheria inasema huwezi kumrithisha mtu wengine wamewarithisha, wengine wameuza, wengine wamebadilisha matumizi na kadhalika. Serikali imeunda kamati inafanya hiyo kazi ikimalizika taarifa kamili tutaitoa.

Nam. 102

Ukosefu wa Kanuni za Mahakama ya Rufaa ya Kodi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kwa muda mrefu Zanzibar kumekuwa na kilio cha kuanzishwa kwa Baraza la Rufaa za Kodi, na bahati nzuri ni kuwa Baraza hilo limeshaanzishwa. Hata hivyo, hivi sasa kumekuwa na tatizo la Kanuni za kuendesha mashauri ya Baraza hilo hazipo, wakati tayari Baraza hilo linafanyakazi, Mwenyekiti wake ameshateuliwa na anaendelea kusikiliza mashauri mbali mbali yanayofika kwake.

Je, ni sababu gani zimepelekea mpaka hivi sasa kutokuwepo kwa Kanuni za uendeshaji mashauri ya Baraza hilo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam.102 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Sheria ya Rufaa za Kodi Nam.1 ya mwaka 2006 imeanzisha Bodi ya Rufaa za Kodi na Mahkama ya Rufaa za

Kodi. Madhumuni ya Bodi na Mahkama ya Rufaa za Kodi ni kushughulikia malalamiko ya walipa kodi dhidi ya maamuzi ya Kamishna wa *ZRB* au Naibu Kamishna wa *TRA*. Bodi hii imeshaanza kazi rasmi tokea mwaka 2013.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi ya kuwa bado Kanuni za uendeshaji wa Bodi hiyo hazijakamilika. Sheria inataka kuwa Kanuni hizo zitayarishwe kwa mashauriano baina ya Jaji Mkuu na Waziri wa Fedha. Tayari rasimu ya kanuni hizo imeshatayarishwa na zinatarajiwa kukamilika hivi karibuni baada ya kutiwa saini na Mhe. Jaji Mkuu, kwa sasa Bodi inaendeshwa kwa Kanuni za mwaka 2007 (*The Zanzibar Tax Appeals Board Rules of 2007).*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa kukiri na huu ndio uungwana. Lakini sheria imekaa muda mrefu kwa Mwanasheria Mkuu kipindi kirefu ikawa napigia kelele huku ndani. Je, ni sababu gani kukaa kwa Mwanasheria muda mrefu sheria hiyo wakati wananchi wanasubiri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini Mhe. Waziri kama hapo hapatoshi akishakutaja hii kama hakutaja wajumbe sheria hii haiwezi kufanya kazi. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa umakini wake aliokuwa nao kama kumshtua tu kataja wajumbe, ili sheria hii hata ukishakuita sheria haiwezi kufanya kazi kama hawajaidhinisha wajumbe. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na ambayo kakiri kutokamilika kwa kanuni. Je, Mhe. Waziri kwa kuwa amekiri kwa

kutokuwepo kwa kanuni zinazosaidia uendeshaji wa Baraza hili la Kodi nataka kuuliza swali lenye (a) na (b).

(a) Kuna changamoto gani zilizopelekea ambazo zinalazimu ukiukwaji wa Kanuni hizo maana lazima kutakuwa na changamoto.

(b) Kuendelea kuendesha chombo hicho bila ya kuwekwa hizo Kanuni hatuoni kwamba tutaendelea kufanya hukumu ambazo tunawadhulumu upande mmoja kwa kutokuwepo kwa kanuni hizo.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwanza ni utaratibu wa kawaida kwamba tunapokuwa na sheria lazima ziwepo na kanuni, kwa sababu kanuni ndizo zinazofafanua *process* nzima au utekelezaji wa hiyo sheria. Kwa hiyo, sheria imetungwa lazima iwekewe kanuni zake na kama zilivyo sheria nyengine, kanuni za sheria hii ni muhimu kwa sababu zitasaidia katika utekelezaji wa sheria yenyewe.

(b) Bodi pamoja na Mahkama zinafanya kazi zake na kama nilivyosema zinafanya kazi zake kwa kutumia Kanuni zilizotungwa mwaka 2007. Kwa hiyo, kazi haijasita kanuni zipo, kinachofanyika sasa hivi kutunga kanuni mpya zitakazoweka utaratibu mzuri zaidi wa kuendesha mashauri ambayo yanapitishwa kwenye Bodi au yanayopitishwa kwenye Mahkama. Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba kanuni hizi zitakamilika ndani ya mwaka wa fedha 2017/2018. *(Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri amesema bodi hii imeanza kazi tokea mwaka 2013. Sasa napenda kujua tu kwamba hadi hivi sasa ni wafanyabiashara wangapi wameshapelekwa huko kwenye hiyo Bodi ya Rufaa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi lenye kutaka kujua ni mashauri mangapi yamepelekwa kwenye bodi.

Mhe. Mwenyekiti, nimueleze tu kwamba kwa taarifa tulizonazo idadi ya kesi zilizowasilishwa ni tisa (9), kesi tano (5) zimepata suluhisho. Kwa maana wengine wamekubali kuzitoa na kuzungumza nje ya Mahkama. Katika hizo tatu (3) zipo kampuni za simu tatu (3), kuna Kampuni ya *Airtel* ambayo tayari imeshalipa bilioni 2, kuna *Vodacom* ambao wamelipa bilioni 1.8 na Tigo na wao wamelipa bilioni 2.

Lakini pamoja na hayo, zipo kesi ambazo zinaendelea kuendeshwa katika Mahkama. Vile vile ninavyojua kwamba tayari kuna kesi ambazo zimepewa *referred* kwenye Mahkama ya Kodi za Rufaa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Kwanza nikupongeze Mhe. Waziri kwa majibu yako. Lakini nilitaka kujua kwa kuwa sheria nyingi zimekosa utekelezaji kwa kuchelewa kutungwa Kanuni. Lakini pia Wawakilishi ni muda mwingi tumekuwa tukilieleza swali hili kwa lugha ile ya kisheria ambayo inaonesha haimlazimishi Mhe. Waziri kutunga kanuni na kipande kile kinasema "Waziri anaweza kutunga Kanuni",

ambapo anaweza akatunga au ama anaweza akawacha kutunga hiyo kanuni.

Swali langu, ni lini serikali itaondosha kile kifungu anaweza na iweke "Waziri atatunga Kanuni" ili sasa hizi sheria zetu tunapozitunga, basi kuwe kuna umuhimu wa kuweza kulazimisha kutunga ile Kanuni ili sheria zetu ziweze kutekelezeka kiurahisi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba kipengele hicho cha kisheria kimewekwa kwa madhumuni maalum na ukizisoma sheria nyingi Mhe. Mjumbe ni kwamba huwa inaainisha maeneo ambayo Mhe. Waziri anaweza kutunga kanuni katika maeneo hayo. Kwa hivyo, sio lazima kama sheria zilivyo ni pale Mhe. Waziri amepewa mamlaka kwamba atakapoona kuna haja ya kufanya hivyo basi afanye hivyo katika yale maeneo yanayolazimika kufanya hivyo, na wakati mwengine sheria zinayaainisha kwamba maeneo haya Mhe. Waziri anaweza kuyatungia kanuni kadri atakavyoona inafaa.

Kwa hivyo, bado nimwambie Mhe. Mjumbe kwamba hicho ni kipengele kimewekwa kwa madhumuni maalum katika sheria zetu na kina sababu maalum. Hivyo, naomba kiendelee hivyo hivyo na serikali isikibadilishe kwa hatua za sasa.

Nam. 108

Uvunjifu wa Sheria za Barabarani kwa Waendesha Vyombo vya Maringi Mawili

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Zanzibar ni nchi moja wapo ambayo wananchi wake wanatumia usafiri wa vyombo vya maringi mawili kama vespa, pikipiki na

kadhalika. Vyombo hivyo hutumika kwa watu wenye rika tofauti ambapo kwa sasa hutumika kwa vijana kuanzia miaka kumi na tano. Vijana hao hutumia zaidi vyombo hivyo kwa kufanya fujo kwenda mbio kupita kiasi ambapo huhatarisha maisha yao na maisha ya watumiaji wengine wa barabara hizo.

(a) Je, serikali hailioni tatizo hili.

(b) Kama inalijua, hatua gani zimechukuliwa kukomesha vitendo hivyo.

(c) Ni lini serikali itapiga marufuku vitendo hivyo ili kupunguza ajali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 108 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Zanzibar wananchi wake wengi wanatumia usafiri wa vyombo vya maringi mawili na kwa mujibu wa kifungu cha sheria nambari 7 ya mwaka 2003 leseni ya udereva daraja (M) hutolewa kwa vijana waliotimia umri wa miaka 16 ambao huruhusiwa kuendesha vyombo vya *moped*, na leseni ya udereva daraja (A) hutolewa kwa vijana waliotimia umri wa miaka 18 ambao huruhusiwa kuendesha vyombo vya maringi mawili vinavyozidi 50 CC.

(a) Mhe. Mwenyekiti, hivyo kuendesha chombo cha moto chini ya umri huo ni kosa na dereva na aliyempa chombo wanastahiki kuchukuliwa hatua za kisheria, kwa sababu wote ni wakosa.

(b) Mhe. Mwenyekiti, serikali kwa kutumia Jeshi la Polisi huwakamata wote wanaobainika kufanya makosa hayo na kuwachukulia hatua za kisheria.

(c) Mhe. Mwenyekiti, serikali imeshapiga marufuku vitendo hivyo na wanaobainika kufanya huchukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria yetu hii.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nataka anipe majibu ya nyongeza kidogo.

Kwa kuwa tukipita barabarani tunakamatwa kama leseni au *insurance* imemaliza muda wake, lakini vitu hivi kama Idara ya Usafiri na Leseni na ndio inayotoa leseni na ndio yenye kuonesha adhabu pamoja na *penalty* yoyote kama utakuwa umemaliza muda wako au kitu gani. Lakini kwa hapa kwetu mambo haya anakukamata polisi baada ya kukamatwa na Idara ya Leseni.

a) Ni sheria gani inayompa polisi kutukamata wakati yeye si aliyenipa leseni.

b) Kwa kuwa unataka kuanzisha adhabu ya kukamatwa kwa vyombo ya papo kwa papo ni Jeshi la Polisi au Idara ya Usafiri na Leseni ambayo itakuwa inatoa adhabu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 (2003) na kwa mujibu wa kifungu 160 Polisi ndio waliopewa jukumu la kushughulikia suala hilo.

b) Tutakapofanya hiyo kazi tutashirikiana vile vile na *ZRB* katika kuhakikisha kwamba faini za papo kwa papo zinatekelezwa kwa ufanisi pamoja na polisi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Swali langu Mhe. Naibu Waziri katika suala la askari ambao wanakamata watu wa bodaboda tunaona kwamba wanashirikiana na wafanyakazi wa Wizara yake ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji lakini wafanyakazi wale hawana mashirikiano mazuri sana kutoka katika wizara yake ingawa wanatoka katika wizara yake. Nimuulize Mhe. Naibu Waziri.

(a) Je, ni mashirikiano gani ya dhati ambayo anawapatia wafanyakazi wale wa Idara ya Usafiri na Leseni ambao wanajitolea katika kuwalinda watu wale wa *T - One* wanaovunja sheria barabarani.

(b) Je, ni motisha gani anayowapatia wafanyakazi wale, ili na wao wapate nguvu ya kufanya kazi zile ambazo ni nzito, zinawaondoshea upendo kwa vijana ambao wanawakamata barabarani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Zulfa Mmaka Omar swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo kazi ya kukamata *T - One* na wengine wote inafanywa na Jeshi la Polisi na wanaendelea kufanya kazi hii vizuri na hivi sasa tumeona *T - One* wamepungua sana. Kwa sababu tumefika hatua sasa kwa kutumia polisi wa majimbo na wa shehia (Polisi Jamii) kuhakikisha kwamba tunawafikia wale walengwa wenye kufanya

hivyo vitendo kule kule majumbani kwao. Kwa hiyo, ni kazi ya Jeshi la Polisi sio ya watu wa usafiri barabarani sisi kazi yetu ni kukagua vyombo, leseni, mambo ya *road license* pamoja na bima kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.
Kuhusu motisha, sisi tutaendelea kutoa motisha kwa pale kazi wanapozifanya na hii kazi kama alivyosema sio ndogo, lakini kila siku tunaendelea kuwashajihisha wafanyakazi wetu kuifanya hii kazi kwa umakini ili wasipokee rushwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kuna vijana au watu ambao wanavunja sheria za barabarani, wanaendesha pikipiki na vyombo vingi vya maringi mawili ikiwemo vespa na vitu vyengine bila ya *sight mirror* na kusababisha ajali. Je, ni vijana wangapi wamechukuliwa hatua na ni hatua gani kali ambazo zimechukuliwa kwa watu hawa wanaosababisha ajali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, nilijibu swali hili juzi niliulizwa na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa. Kwa mujibu wa kifungu chetu cha 202 sisi kazi ya Jeshi la Polisi ni kumchukua yule muhusika kumpeleka Mahkamani na baadaye kumpiga faini ambayo haipungui US$ 150 na zile pesa zinazopatikana baada ya kuonekana na mashtaka zinaingia katika Hazina ya Wizara ya Fedha. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 149

Uharibifu wa Viwanja vya Michezo

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini - Aliuliza:-

Imekuwa kawaida siku hizi kwa wanafunzi wa udereva kujifunza katika viwanja vya Maisara.

(a) Kwa nini, wizara yake inaliachia suala hilo kuendelea na kuharibu viwanja vya michezo.

(b) Hatua gani wizara yake itachukua kudhibiti vitendo hivyo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 149 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba wizara yangu kupitia Idara ya Usafiri na Leseni ndiyo yenye kutoa ruhusa kwa *Driving Schools* kuwafundisha wanafunzi gari pamoja na vyombo vyengine vya moto. Hatahivyo, walimu hao hawapewi ruhusa ya kufanya mazoezi ya udereva katika viwanja hivyo vya michezo na wamiliki wa viwanja hivyo wanayohaki ya kuwazuiya, ili wasiharibu viwanja hivyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu itawaarifu wahusika kuacha kuvitumia viwanja vya michezo kwa kuwafundisha wanafunzi wao katika maeneo hayo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kukiri kwamba kwa kweli hawa wenye skuli hizi za kufundisha udereva wa gari hawapewi ruhusa ya kufanya mazoezi katika viwanja vile vya Maisara, ambapo kwa kweli wanakera vijana wetu kufanya

mazoezi ya mpira wa miguu hata na *golf* na michezo mingine. Sasa kama ni hivyo, kwanini basi hashirikiani pamoja na hiyo taasisi ambayo wenye viwanja tunawajua ni Baraza la Manispaa la Mjini, ndio wenye viwanja na wao hasa ndio dhamana tunavyofahamu, sijui kama kuna mabadiliko mengine. Kwa nini, hawashirikiani kuwakamata *on the spot* papo kwa papo. Lakini ukisema utawapa onyo au atawafuatilia unajua tena mambo yetu, kwa kweli kama wanawaona wawakamate tulidhibiti lile suala kabisa. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza. Sisi tuna mashirikiano mazuri pamoja na watu wa Manispaa na Tawala za Mikoa wote na Polisi katika masuala yote. Iwapo hawa watu sisi tunawajuwa kwamba, wanavyotakiwa kuwaruhusu kufanya mazoezi katika *open space*, katika viwanja kama nilivyosema hili haliruhusiwi ni wajibu wao kuwakataza wenye viwanja vyao wasivitumie na wanaweza kukaa nao na kuzungumza nao kuhusu suala hili. Vile vile, tunaweza tukaangalia kanuni zetu namna gani ya kuliangalia hili suala kwa hapo baadaye. Lakini sisi tunapenda sana kila wenye vyuo wawe na sehemu zao maalum za kufundishia.

Tunawapongeza sana Jeshi la Polisi kwa sababu wao wana sehemu kubwa mle ndani Ziwani na ndio maana wanaweza kutoa *class* zote za udereva kutokana na kwamba wao wana *space* yao. Kutokana na hali hiyo, nawaomba wengine watafute sehemu ambazo haziingiliani na majukumu ya watu wengine. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo saa la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri. Lakini kwanza nimpongeze kwa majibu mazuri ya swali mama aliyojibu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri haoni sasa umefika wakati wa kuweka sharti kwa vyuo hivi vinavyofundisha udereva kuwa na maeneo yao ya mazoezi. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nalichukua swali lake na tutalifanyia kazi.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu ya serikali yenye kigugumizi naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa sababu mtindo huu tayari unaendea katika viwanja mbalimbali vya michezo na kwa kushirikiana wizara yake na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo inasema nini serikali kudhibiti hasa kwa kuwapiga faini moja kwa moja watu hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza. Kama nilivyosema Mhe. Waziri ana uwezo wa kutunga kanuni kama nilivyomjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi tutakaa na wahusika tulijadili suala hili ili wasiingilie katika viwanja ambavyo havina haki na wao. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 88

Mikakati ya Kuimarisha Soka Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Hivi karibuni Zanzibar imeshuhudia nguvu mpya ya kuimarisha soka Zanzibar baada ya kuanza mashindano ya Majimbo (*Majimbo Cup*), ambayo yalifunguliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed

Shein. Katika uzinduzi wake Mhe. Rais alipongeza Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuyafadhili mashindano yale ambayo yeye mwenyewe ni Mwenyekiti.

(a) Je, mbali na mkakati huu mzuri wa kuimarisha soka visiwani serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mpira wa miguu Zanzibar unapiga hatua katika ngazi zote za ligi.

(b) Je, kwavile muda mrefu kumekuwa na matatizo ya uongozi katika vyama vya mchezo wa soka Zanzibar. Serikali haioni ni muhimu sasa kuwaita wahusika wote na kukaa nao pamoja na wataalam mbalimbali, ili kuweka dira ya mchezo wa mpira wa miguu hasa katika uongozi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, serikali kwa kushirikiana na Chama cha Mpira wa Miguu kitahakikisha ligi inachezwa na kusimamiwa vilivyo kulingana na Kanuni za michezo husika.

(b) Mhe. Mwenyekiti, hakuna mgogoro wowote wa Uongozi katika Chama cha Mpira cha Zanzibar. Kutokana na sababu hiyo ndio maana tumekubalika kuwa mwanachama wa *CAF*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, mimi nataka kumwambia tu Mhe. Naibu Waziri, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii naomba ku-*declare interest*. Mhe. Mwenyekiti, huu ni Mwezi Mtukufu wa

Ramadhan unakaribia kumalizika hili jawabu kanuni zetu zinatukataza, tumekaa na Wajumbe wa Kamati wenzangu mashahidi mgogoro upo. Hata katika mchango wetu juzi nimesema na Maalim mwenyewe Waziri kakiri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba uulize swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Waziri nikishamthibitishia tatizo hili yupo tayari kujiuzulu nafasi yake kwa kushindwa kusimamia ukweli kwa mujibu wa kanuni zetu. Yupo tayari kujiuzulu kuhusu tatizo hili na hili tatizo lipo, tumekaa mimi na yeye shahidi kuna mgogoro kati ya *ZFA* na Baraza la Michezo sasa anakuja kujibu nini humu ndani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nilijulishe Baraza kwamba nakiri Mhe. Jaku Hashim Ayoub ni Mjumbe wa Kamati yetu ya Habari na Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, yeye Mhe. Jaku Hashim Ayoub atakuwa ni shahidi tumekao nao pamoja watu wa *ZFA* pamoja na Baraza la Michezo na wao wakaahidi mbele ya kamati kwamba watahakikisha migogoro hii imeondoka na kuendeleza mpira wetu kama kawaida. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

UTARATIBU

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu 63 kuhusu utaratibu, 37 Mheshimiwa...

Mhe. Mwenyekiti: 63 Mhe. Jaku Hashim Ayoub, 63 nimekuruhusu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu baada ya 63 inakuja 37.

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu utaratibu kanuni gani imevunjwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Labda nikusomee Mhe. Mwenyekiti, kifungu 63 taarifa kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: 63 nimekuruhusu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Taarifa kuhusu utaratibu baada ya hapo nakuja kifungu cha 37

Mhe. Mwenyekiti: Taja kanuni iliyovunjwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: 37 Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme utaratibu kisha nakuja na kanuni yenyewe kwa mujibu wa kitabu chako hiki.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku naomba ukae tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa Baraza linapotoshwa hili.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mwenyekiti, pamoja na majibu yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri kadhia

nzima ya mkakati wa kuimarisha soka Zanzibar. Pamoja na migogoro aliyoikataa. Je, ni taratibu gani zilizopelekea ndani ya migogoro hiyo baadhi ya wajumbe wanaoshiriki katika Chama cha Mpira wa Miguu kufungiwa maisha wasishiriki katika chama hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa kuwa ni mwanamichezo mzuri na anafuatilia taarifa mbali mbali za michezo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba tu nimjibu Mhe. Mjumbe kwamba taratibu ambazo zilipelekea baadhi ya viongozi hawa kufungiwa maisha naomba kwamba kuna sheria, taratibu na kanuni ambazo Chama cha Mpira wa Miguu wanazifuata.

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba hawa watu ambao wamehukumiwa hukumu hiyo ya kufungiwa maisha zipo taratibu walalamike na kuna Kamati ya Usuluhishi na Rufaa kama hawakuridhika na uamuzi huu basi wakate rufaa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa sababu ametaja kanuni mbali mbali na kwa kuwa mwanzo alikiri hakuna migogoro lakini baadaye amekiri kuwa kuna watu wamefungiwa maisha. Ni kanuni ipi ambayo *ZFA* inaifuata ya kuweza kuwafungia viongozi wake maisha.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Lakini kabla ya kumjibu swali bado niendelee kumpongeza Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kuweza kujibu maswali kama vile inavyotakiwa kuyajibu. Nikiendelea na kumjibu swali lake Mhe. Abdalla Maulid Diwani ni kwamba *ZFA* inafuata katiba na kanuni zake ambazo zinafuatwa na vyama vyote vilivyosajiliwa na chama hicho, kwa mujibu wa kanuni ziliopo na kwa mujibu wa katiba iliopo ndio inayopelekea kutoa adhabu kwa mujibu wa kosa lilivyo. Kutokana na hilo basi, kanuni zilizotumika ni zile zinazofuatwa na *ZFA* na hao *ZFA* ndio wametoa hizo hatua za kuchukua kwa wale ambao wamefanya makosa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri swali litaulizwa na Wizara hiyo hiyo na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Jimbo la Paje.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali ilivyo kama hivi na ajabu hii na uwezo huu na umakini wenyewe ndio huo. Naomba kuondosha swali maana yake nitapoteza muda bure.

Nam. 185

Ubovu wa Ubao wa Magoli (*Score Board*) katika Uwanja wa Gombani

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)

Nam. 175

Wanafunzi Waliopata Mimba Unguja na Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Hivi karibuni kumekuwa na taarifa za kuongezeka vitendo vya kupata mimba wanafunzi ambavyo vinaathiri maendeleo ya wanafunzi hao Unguja na Pemba.

Je, ni wanafunzi wangapi wamepata mimba Unguja na Pemba na wizara imechukua hatua gani kwa wanafunzi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 175 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, udhalilishaji wa watoto ni tatizo ambalo linakuwa na kuongezeka siku hadi siku hapa Zanzibar. Afisi ya Mrajis wa Elimu ndio sehemu pekee katika wizara yangu inayoshughulikia kesi hizi kwa kuweka kumbukumbu sahihi kwa kesi zote ambazo huripotiwa Katibu Mkuu kutoka skuli zinazohusiana na masuala ya kesi za ujauzito kwa wanafunzi.

Takwimu zilizoripotiwa kwa mwaka 2016/2017 zinaonesha jumla ya kesi za ujauzito ni ishirini na sita (26) kwa Unguja na Pemba.

Hatua zilizochukuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kukabiliana na tatizo la wanafunzi kupata ujauzito ni kama zifuatazo:-

i. Kufanya uhakiki kujua kiwango halisi cha kesi hizi zilizojitokeza katika skuli zote za Unguja na Pemba kwa mwaka 2016, badala ya kukaa afisini na kusubiri kuripotiwa sambamba na kuwafahamisha Walimu Wakuu umuhimu wa kuziripoti kesi hizi.

ii. Kuendelea kuziripoti kesi hizi kwa Makamanda wa Polisi katika maeneo ambapo matokeo haya yanatokea, pamoja na kufuatilia kwa karibu hatua za kiuchunguzi na kuwashtaki watuhumiwa.

iii. Pia, wizara inawaruhusu wanafunzi kuendelea na masomo na kutokana na marekebisho yaliyofanywa na Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto ya mwaka 2005 kifungu cha 20(4) cha Sheria ya Elimu. Kifungu hiki kimerekebishwa katika Sheria ya Kuwalinda Wari na Mtoto na Mzazi mmoja ya 2005 kifungu 4(1), (2). Kifungu hiki kinaeleza kuwa:

> "Endapo msichana anapatikata ujauzito wakati bado ni mwanafunzi anaweza mara moja kusimamishwa skuli na anaweza kurejeshwa tena skuli katika mwaka wa masomo unaofuata kufuatia kujifungua au wakati mwengine wowote utakaoonekana unafaa na taasisi ya elimu, lakini kwa hali yoyote ile usimamishwaji hautazidi miaka miwili ya masomo".

Aidha, wizara pia imekuwa ikichukua hatua nyengine kukabiliana na suala hili ikiwa ni pamoja na kuwakumbusha walimu kufuatilia nyendo za wanafunzi katika maeneo ya skuli au karibu na skuli. Lakini pia hatua nyengine ni kuzishirikisha Kamati za Skuli kuwakumbusha wazazi kuwafuatilia nyendo za watoto wao. Aidha, walimu huwa wanatoa mawaidha kupitia hadhara mbali mbali za wanafunzi juu ya kujitambua, kujienzi, kujilinda, kujihifadhi na pia wakati mwengine kukemea kulaani vitendo hivi vya kishetani. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Lakini tu Mhe. Mwenyekiti, tunavyouliza serikali sifikirii kama tunamkomoa mtu tunafanya kazi kwa wajibu wetu. Namuona Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf sasa hivi katulia kabisa naona hili zogo haliwezi kwa majibu kama haya na mimi nitafika pahala haya majibu nikae upande nisilete tena maswali kwa hali kama hii. Unauliza njia ya kwenda Uwanja wa Ndege huku anakwambia mtu upite Bububu hatuwezi kufika hivi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, napenda kuuliza swali dogo la nyongeza.

a) Katika kesi hizi za kadhia ya mimba walimu wangapi wamehusika katika vitendo hivi.

b) Hicho kifungu alichokitaja Mhe. Naibu Waziri haoni kinazidisha au kinapunguza matatizo hayo, hebu akiangalie vizuri Mhe. Naibu Waziri kutokana na elimu yake aliyokuwa nayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwa mujibu wa ripoti tulizonazo katika kesi hizi 26 hakuna mwalimu hata mmoja ambaye amehusishwa na shughuli hizi. *(Makofi)*

b) Kifungu hiki ambacho kinaruhusu kufuatia maslahi ya kidunia juu ya haki za binaadamu kwamba pamoja na tatizo alilopata kijana ikaonekana si sahihi tena kumfukuza skuli, kwa hivyo Sheria yetu ya Elimu bado inasisitiza kufukuzwa mwanafunzi. Lakini kuna Sheria nyengine ya Kuwalinda Watoto hii bado

inatetea wanafunzi waendelee kutumia na sisi sasa hivi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunafanya mapitio ya Sheria yetu ya Elimu ya mwaka 1982, ili nayo pia isipingane na Sheria hii ya Kuwalinda Wari na Watoto. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kuniona. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ningependa nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwanza karibuni tumesikia kauli ya Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akihamasisha Watanzania juu ya hasa wanafunzi ambao pia wanaopokea mimba baada ya kujifungua warudi skuli.

a) Lakini nataka kujua nini kauli ya serikali katika uhamasishaji juu ya kauli hii aliyoitoa Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Katika uhamasishaji wa moja kwa moja katika kuhakikisha kwamba hawa vijana wetu wanapokea mimba na wanatakiwa kurudi skuli. Ni utaratibu upi unaotumika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kwamba kunatolewa elimu na maelekezo hasa kwa wazee, ili kulinda maslahi ya watoto wetu kwa ajili ya maisha yao ya baadaye. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ningeomba hili swali la mwanzo alirejee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai Mohammed Said rejea swali la mwanzo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, swali la kwanza nilisema hivi kwamba ambalo lilikwenda sambamba na

swali la kifungu (a) na (b). Ni karibuni kwenye vyombo vya habari ukisoma utaona Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa akizungumza kwa kusikika pia kwamba umuhimu wa watoto wetu wanaopokea mimba baada ya kujifungua hasa wanafunzi waweze kurudi skuli. Sasa katika utaratibu huu inaelekea kwamba tayari kuna kampeni maalum inayofanywa au kutilia uzito jambo hili. Kwa hiyo, nataka kujua pamoja na majibu aliyotoa Mhe. Waziri, nini msimamo wa SMZ katika kauli hii, kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Nafikiri sasa hivi atakuwa kanifahamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake la nyongeza kama ifuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaliona suala hili kwamba ni njia sahihi kabisa ya kuwarejesha vijana wetu hao ambao wamepata ujauzito, na kwa kuwa kesi hizi sio kubwa sana kwa mujibu wa takwimu yetu ni 26 ni kwamba sisi utaratibu huu upo zamani na unaendelea na utaendelea. *(Makofi)*

Tunaelewa kwamba vijana hawa wana haki yao ya kusoma, ispokuwa wamepata mtihani hapa kati kati. Kwa kuona hilo basi na sisi tutandelea kuwashajihisha vijana ambao kwa bahati mbaya watapata mtihani huu waweze kurejea na tunao na wanaendelea kurejea.

Lakini suala hili hili ni kwamba wizara ina Kitengo maalum ambacho kinatoa Ushauri Nasaha wa wazazi na wanafunzi hawa kuweza kurejea skuli, ushauri huu unafanywa kwa siri kubwa, ili kuficha pengine wanafunzi wengine wasielewe kwamba labda

kijana fulani wa skuli fulani amepata tatizo fulani na baadaye akanyanyapaliwa.

Kwa hivyo, tunafanya kwa siri kubwa sana na wakati mwengine kama anahisi skuli 'A' ndiko ambako mwanafunzi huyo anasoma, basi humuhamisha skuki 'B', ili wanafunzi wenzake wasielewe kama amefanya kitendo gani. Kwa hiyo, ushauri nasaha tunatumia sana pamoja na wazazi na watu wengine wote na Walimu Wakuu pia tumewaelekeza na wanafanya kazi hiyo. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pia naomba kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwanza nilitaka kujua wanafunzi wa kiume ambao wanawapatia ujauzito wanafunzi wa kike ni wangapi.

b) Ni hatua gani za kisheria zilizochukuliwa katika kuendelea wao na masomo yao vijana hawa wa kiume.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mpaka sasa ripoti tulizonazo hazijahusisha wanafunzi wa kiume badala yake zinahusisha watu wengine katika jamii.

b) Ni kwamba hatua zinazochukuliwa, kwa sasa hatuchukui hatua yoyote kwa wanafunzi kwa sababu hakuna wanafunzi wanaume waliohusika, lakini wote waliohusika na vitendo hivi wanaripotiwa katika Jeshi la Polisi na wanafanya kazi zao za kiuchunguzi na kisha wanapeleka katika sehemu zinazohusika. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali hili Nam. 171 naomba ku-*declare interest* kama ni Mjumbe halali wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii na nipo makini kusikiliza jawabu kutoka kwenye serikali kuhusu swali hili.

Nam. 171

Malalamiko ya Wafanyakazi wa Kituo cha Kulea Watoto Mazizini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wafanyakazi wa Kituo cha Kulea Watoto cha Mazizini kuwa Mkuu wa Kituo hicho amekuwa anatumia lugha mbaya kwa wafanyakazi waliopo hapo na kurudisha nyuma *morality* ya kazi ya watumishi hao.

Je, wizara haioni kuwa jambo hili linaleta kasoro ya kiutendaji kwa wafanyakazi wa kituo hicho muhimu kwa malezi ya watoto.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa pumzi zake na asubuhi nikaweza kusimama hapa nikiwa na afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 171 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu pamoja na mimi binafsi tunasikitika sana kupokea taarifa hii. Kwani Mkuu wa Kituo

aliyepo ni mtumishi muadilifu, mwenye nidhamu, msikivu, mwenye kujali dhamana zake za kazi na pia mashirikiano mazuri na uongozi, wafanyakazi wenzake na hata kwa watoto anaowasimamia. Tokea kuajiriwa hajapata kuandikiwa aina yoyote ya karipio hata onyo la mdomo, si mtu mwenye kiburi wala majivuno. Kwa masikitiko kabisa limetushangaza sote. Lakini tunachoelewa ni kwamba tokea kuwepo kwake katika nyumba hiyo ametengeneza mahusiano mazuri baina ya wafanyakazi na kiwango cha matunzo kwa watoto kilichoongeza furaha na upendo kwa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haina uhakika na ushahidi wa jambo hilo, lakini kama limetokea ni vyema Kanuni za Utumishi wa Umma kufuatwa. Hata hivyo, suala hili tutalifuatilia tuone ukweli wake na endapo limetendeka Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 itachukua nafasi yake. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nili-*declare interest* mapema nikawa nipo makini nikarudia mara ya pili kusikiliza swali hili. Mimi si mkamilifu na nahitaji msaada wa kila mtu, na uungwana ni vitendo. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii na Mhe. Naibu Waziri alitanguliza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na kamuweka mbele kwanza. Lakini kadhia nimeshachangia na *hansard* hizi hapa ninazo katika bajeti, siwezi kuja kumsingizia mtu tu kitu ambacho hakina uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, yupo tayari Mhe. Naibu Waziri kumletea watu kupokea ushahidi na achukue hatua. Kilichofanyika hapa Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitaka mashirikiano kwa Bi. Saada ndiye mlezi wa mwanzo kutoa mashirikiano kwenye kamati yule bibi kahamishwa, ndio chanzo hiki cha mgogoro hata ikaingia ile kesi ya yule mtoto aliyetoroshwa na wizara, ndio mgogoro wote huu. Kwa nini bibi kashirikiana na kamati akahamishwa akaletwa bibi

mwengine, sasa imekuwa kama ngazi yao. Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kufanya kazi kama hivi…

Mhe. Mwenyekiti: Swali Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, yupo tayari Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Waziri mwenyewe mwenye dhamana kupokea ushahidi, ikisha sijui wataweka wapi kauli yao kama wafanyakazi wataogopa na wala wasiende kuwatisha wafanyakazi mle ndani tupo katika kujenga taifa sisi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Kwanza nataka nimfahamishe Mhe. Mwakilishi kwamba mimi mwenyewe baada ya kupokea suala hili nilifanya ziara katika kituo kile nikazungumza na wafanyakazi, nikazungumza na watoto na nipo tayari kufuatana na yeye kwenda kuwasikiliza hao anaosema yeye na kama sheria itabainika kuna tatizo lolote kama nilivyojibu kwenye jibu langu mama, kwamba Sheria ya Utumishi wa Umma itafuatwa. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nipo katika Nyumba ya Kulelea Watoto Mazizini. Kulikuwa kuna kadhia ya yule mtoto kubakwa ndani ya mikono ya serikali, yaani Nyumba ya Watoto pale Mazizini. Je, ile kesi imefikia hatua gani, japo iko Mahkamani hatulizungumzi nataka mustakabali wa kesi imefikia hatu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa

ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Kama yeye alivyotanguliza kusema kwamba japo iko Mahkamani na mimi napenda kumjibu kwamba kesi hii iko Mahkamani na sisi hatupaswi kuingilia tunasubiri jibu la Mahkama. (*Makofi*)

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 61(3) nakazia Kanuni ya 37, Waziri anapaswa kujibu kwa umakini na ufupi swali lililoulizwa. Nimeuliza iko Mahkamani kweli hatua inasikilizwa, bado haijasikilizwa sijazungumza aongezee yako ndani ya Mahkama, nimeuliza hatua. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa majibu mazuri yametolewea na Mhe. Naibu Waziri ningeomba kuendelea kutoa ufafanuzi kwa maelezo ya Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kanuni zetu 37(3), kifungu cha 9 kinasema hivi:

"Linalohusu jambo lolote ambalo wakati huu liko mbele ya Mahkama maana yake lolote lililoko mbele ya Mahkama haliwezi likazungumzwa hapa, kwa sababu kifungu 37(3) kinasema suala linalohusu jambo lolote kati yafuatayo halitaulizwa au kujibiwa katika Baraza kama linahusu jambo lolote ambalo wakati huu liko mbele ya Mahkama".

Mhe. Mwenyekiti, sasa yeye wajibu wake ni kumuuliza Mrajis wa Mahkama ile kesi imefikia wapi sio humu ndani. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona kwa swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti, sisi Tanzania pia ni wanachama wa nchi za Umoja wa Afrika, lakini pia wa Umoja wa Nchi za Afrika Mashariki ambao ni *East African Community*. Nilitaka kufahamu ni utaratibu upi ambao serikali unautumia kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu hasa katika sehemu hii wanaosimamia juu ya kulea watoto wetu wanajifunza kwa matendo pamoja na nchi za jirani, ili kuhakikisha kwamba vipaji vya watoto wetu hawa ambao ni mayatima na wanalelewa katika hizi nyumba vinaweza kutambulika na kuheshimika kwa upande wa dunia. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu ipo karibu sana katika kuhakikisha wale wote wanaofanya kazi katika nyumba za watoto wanapata elimu na matunzo mazuri kwa ajili ya kuwalea watoto wale yatima.

Lakini, tupo karibu sana na nchi za jirani ambao wanatusaidia katika kupata elimu na matunzo zaidi kwa wafanyakazi ambao wanawahudumia watoto wale katika nyumba za watoto mayatima. *(Makofi)*

Nam. 179

Matatizo ya Maji ya Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya imepitisha bajeti yake juzi na Mhe. Mahmoud Thabit Kombo amejitahidi kutoa hoja sana kwa baadhi ya wajumbe na isije ikaonekana kwa kuwa labda tumefanana mimi na yeye aaa. Ni

kwamba amefanya kazi kwa mazingatio makubwa ya wananchi, isije ikaonekana kama nataka kumpendelea naomba kuliondosha swali hili kwa kazi aliyoifanya Mhe. Waziri, nampongeza kwa dhati.

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

UTARATIBU

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 40(4). Mhe. Mwenyekiti, siku ya tarehe 03/06/2017 niliuliza swali linalohusu jambo la nyaraka na kwa sababu hiyo hiyo sijapata jawabu. Kama kanuni hii inavyosema ni siku tatu kwa maandishi sasa nataka kujua je, wizara imeweza kupeleka Ofisi ya Mhe. Spika taarifa ya kuongezwa kwa siku ili wajibu swali hili au hawajajibu. Pamoja na kujibiwa vijembe vingi na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ni mtindo mkubwa wa mawaziri kutujibu vijembe naomba swali langu hili uliweke vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohammed Said Mohammed nimekufahamu kuhusu utaratibu wa Kanuni hiyo ya 40(4). Kwa taarifa tu kuwa Ofisi ya Spika haijapata taarifa yoyote au barua yoyote kuhusiana na swali hilo. Lakini nilikuwa naomba sana niwakumbushe tena mawaziri na mara nyingi kiti kinakumbusha kuwa maswali yale yanayoahidiwa kwa maandishi waifuate ile Kanuni ya 40(4) walete majibu ya maswali hayo kwa muda usiozidi siku tatu. Lakini nilikuwa naomba niseme kwamba waziri anayehusika hapa simuoni, nilikuwa namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alifuatilie suala hilo ili hayo majibu yapatikane. Ahsante.

Waheshimiwa Wajumbe, katika *order paper* yetu ya leo shughuli zilizopangwa zimemalizika. Kwa hiyo, kabla ya kuakhirisha

naomba nitoe taarifa kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali. Waheshimiwa Wajumbe, tunakumbushwa kwamba Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 itasomwa kesho kutwa Jumatatu tarehe 12/06/2017 wakati wa saa 3:00 asubuhi. Hivyo, kwa taarifa hii nawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri kuwakumbusha Makatibu Wakuu wao kuhusiana na uwasilishaji wa bajeti hiyo.

Aidha, tayari maafisa wetu wanasambaza kadi za mialiko kwa ajili ya shughuli hiyo kwa Makatibu Wakuu hao pamoja na waalikwa wengine wakiwemo Mabalozi wadogo na wawakilishi wa Taasisi za Kimataifa zinazofanya kazi hapa Zanzibar, Viongozi wa Vyama vya Siasa, Viongozi wa Dini na viongozi wengine wa baadhi ya Taasisi za Serikali, waalikwa wote wanaombwa wawe wameshafika katika nafasi zao wakati wa saa 2:30 asubuhi. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wajumbe, nachukua fursa hii kwa kuwashukuru sana nyinyi kwa utulivu wenu pamoja na mawaziri kwa majibu mliyotoa. Lakini niongeze tena kusisitiza kwa kutumia hicho kifungu cha 40(4) yale maswali ambayo Waheshimiwa Mawaziri mnatakiwa myalete kwa maandishi mkipitie hicho kifungu ili mlete hayo majibu yasije kuleta mzozo kwa Waheshimiwa Wajumbe ambao wameuliza maswali hayo. Naomba niakhirishe kikao mpaka Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

(Saa 4:25 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 12/06/2017 saa 3:00 asubuhi)